JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME.

SHULE YA SEKONDARI KASEMPOMBE,
S.L.P 217,
SAME.
15/12/2020.

MKOA WA KILIMANJARO,
KUMB.NA.KSS/A1/30/JIF/2021

JINA LA MWANAFUNZI ……

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASEPOMBE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.</u>

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya kutwa Kasempombe mwaka 2021 . Shule hii inachukua Wanafunzi wa jinsia mchanganyiko . Nakupongeza kwa dhati kuchaguliwa kwako na karibu sana kwenye Shule yetu. Utatakiwa kusoma kwa makini maelezo ya fomu hii, kisha utajaza viambatanisho vilivyoambatanishwa ambavyo ni:

- ✓ Fomu ya mkataba wa kujiunga na Shule, Ijazwe na Mzazi na Mwanafunzi kisha irejeshwe Shuleni.
- ✓ Fomu ya kuthibiti afya ijazwe na Mganga wa Hospitali ya Wilaya (Serikali) kisha irejeshwe Shuleni.

1. KUFUNGUA SHULE:-

- ➢ Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 siku ya Jumatatu. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni saa moja kamili(1:00) asubuhi akiwa na mzazi/mlezi wake. Mwanafunzi atakayeripoti bila mzazi/mlezi hatapokelewa. Muda wa kuripoti shuleni ni siku mbili (2) tangu siku ya kufungua shule.

2. MAHALI SHULE ILIPO:-

- ➢ Shule ipo Wilaya ya Same, Kata ya Mwembe, Kijiji cha Mwembe, Kilomita kumi na tano (15km) kutoka Same Mjini. Iwapo unakubali nafasi hiyo ni muhimu ufuate taratibu zifuatazo kabla ya kujiunga na shule hii.

1. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA KUTOKA KWA MZAZI:-

1 : SARE ZA SHULE (Kitambaa kizito)

i) Kila mzazi/ Mlezi amwandalie mwanaye suruali mbili (2) za rangi ya **Kijani Kibichi** kwa wavulana na mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi yenye mfuko mmoja upande wa kushoto. NB:Mwanafunzi atakayeshona suruali **modo/ kichupa** hatapokelewa shuleni ***Haziruhusiwi***.

ii) Kwa wasichana sketi mbili ndefu (2) za rangi ya **Kijani Kibichi** zenye mshono wa rinda box na mashati meupe mawili (2) ya mikono mifupi yenye mfuko mmoja upande wa kushoto

iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi kwa wavulana na wasichana

iv) Mwanafunzi aje na sweta rangi **Kijani Kibichi** kwa wavulana na wasichana

v) Soksi jozi mbili (2) za rangi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana

vi) Rangi ya ijabu ifanane na sare za shule (Onana na uongozi wa shule kwa maelezo zaidi)

2. MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU HAPA SHULENI:-

i) Mwanafunzi aje na madaftari kumi kwa ajili ya masomo yake (Counter Book Q3)

ii) Kalamu ya wino na penseli

iii) Mkebe wa hesabu (Mathematical set)

iv) Kamusi ya Kingereza (Dictionary ndogo ya Oxford)

v) Vifaa vya usafi (ufagio wa chelewa, jembe) kwa wavula na (ufagio na chelewa na fyekeo) kwa wasichana)

3 . SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu No. 25.

(3A) HESHIMA:-

a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(3B): Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Nimarufuku kuwa na simu ya mkononi au Ipad.

4. CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI

- Kikao cha wazazi cha tarehe 29/11/2019 tulikubaliana kuwa Wanafunzi wote tatakiwa kula kwa kuchangia vitu vifuatavyo**:**

- Kande kg 12 kwa muhula
- Maharage kg 4 kwa muhula
- Pesa ya Mpishi, Chumvi, Mafuta Steel Wire, Sabuni nk. Sh. 7,500 kwa muhula.

NB: Vitu vyote hivi vitakusanywa siku ya kufungua shule , kila Mzazi azingatie kwani wajumbe wa kamati ya chakula na taaluma watakuepo Shuleni tarehe kuanzia tarehe 11 - 15/01/2020 kwa ajili ya kupokea michango na chakula.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Chalse M Antipas

……

MKUU WA SHULE

FORM NA. A.

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

SHULE YA KASEMPOMBE SEKONDARI

S.L.P 217,SAME.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.

1.Mimi:_____MS/MV_(*majina matatu)* Nimeafiki kujiunga na shule ya Tae sekondari.Ninaahidi kusoma kwa bidii na kufuata sheria zote za shule na sitaleta usumbufu wowote KWA WALIMU NA WAZAZI NIWAPO SHULENI.
JINA:_____[KUTWA/HOSTEL]SAHIHI:_____TAREHE:-_____
(MWANAFUNZI)
WA KIJIJI CHA:_____KATA YA :_____RAIA WA:_____

2.Mimi:(majinamatatu)_____(mzazi/mlezi)wa:_____

KIDATO CHA:_____MWAKA**:_____**
WA KIJIJI CHA:_____KATA YA :_____RAIA WA :_____
KAZI YANGU NI:_____ANUANI YANGU NI:_____
Nakubali kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kufuatilia maendeleo ya shule , ya mwanangu na kutekeleza wajibu wangu kama mzazi. JINA:_____SAHIHI:_____TAREHE:_____
NAMBA YA SIMU:_____

>NDUGU WA KARIBU (MLEZI): MAJINA:_____ANAPOISHI:_____
ANUANI:_____ NAMBA YA SIMU:_____

3.UTHIBITISHO WA URAIA.
MIMI:_____MTENDAJI WA KIJIJI/KATA YA:_____

Nathibitisha kuwa M/FUNZI:_____KID>:_____mwaka:_____

NI MKAZI WA KIJIJI CHA:_____KITONGOJI CHA:_____NA NI/SI MTANZANIA,

NI RAIA WA: _____

_____
MHURI NA SAHIHI NA TAREHE (MTENDAJI WA KIJIJI/KATA

FORM B

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To Medical office:

.....

.....

Name of student: .....

Please examine the above named student to ascertain her fitness for Secondary School Education.

Pregnancy will render a female student ineligible of the studies.

Date: ....
Signature

(Headmaster/Headmistress)

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed a government medical officer)

I here by examined the above named student and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for admission.

a) Eye sight .....
b) Hearing .....
c) Limbs .....
d) Speech .....
e) General diseases .....
f) Leprosy .....
g) Epilepsy .....
h) Neuroses .....
i) Pregnancy .....
j) Skin .....
k) Blood .....
l) Chest .....

m) Abdomen .....
.....
n) Spleen .....
.....
o) Other serious disease.....
.....

Comments / Remarks: .....
..

Date: .....
Signature: .....

Station: .....
Designation: .....

Delete unnecessary